

Jibu: Turejee...

Walawi 7:9 “Na kila sadaka ya unga iliyookwa MEKONI, na yote yaliyoandaliwa chunguni, au kaangoni, yote yatakuwa ya huyo kuhani aliyeyasongeza”.

Mekoni ni jiko la kuokea mikate kwa lugha ya kiingereza ni “oven”.

Katika agano la kwanza sadaka zote za unga zilizotengenezwa kwa kupikwaBwana Mungu aliagiza ziwe ni riziki za makuhani wanaofanya kazi yake katika nyumba yake.

Walawi 7:10 “Na kila sadaka ya unga, kama umeandaliwa na mafuta, au kama ni mkavu, watautwaa wana wote wa Haruni kuutumia, kila mtu sawasawa”

Katika agano jipya pia Bwana ameruhusu wanaohudumu madhabahu wale kupitia madhabahu..

1 Wakorintho 9:13 "Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu?

14 Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili"

Unapotoa riziki kwa wanahubiri injili unafanya jambo lenye thawabu kwasababu ni maagizo ya Bwana na si sheria.

Shetani kaliharibu hilo eneo la matoleo na kuwafanya watu wasitoe kabisa wakiamini kuwa ni biashara zinafanyika..

Ni kweli wapo wanaofanya injili kama biashara lakini si wote, hatuwezi kuacha kutimiza majukumu kwa Bwana kwasababu ya uharibifu wa shetani, tutaendelea mbele kwasababu Ukristo ni mapambano.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Mekoni ni wapi? (Walawi 7:9).

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

*NIMEYATUNZA MANENO YA KINYWA CHAKE ZAIDI YA RIZIKI
YANGU.*

*YANAYOENDELEA SASA KATIKA MADHABAHU YA MUNGU
ROHONI.*

MADHABAHU NI NINI?

Mekoni ni wapi? (Walawi 7:9).

Tofauti kati ya makuhani na walawi ni ipi?

VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 1

Share on:

WhatsApp